



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MADARASA 47 KATIKA MANISPAA YA

SINGIDA KUPITIA MRADI WA BOOST HADI TAREHE 23 JUNI 2023

Halmashauri ya Manispaa ya Singida imepokea fedha za ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishai ambapo kiasi cha Tshs. 1,371,500,000 zimepokelewa kupitia mradi wa BOOST.

Taarifa ya utekelezaji ni kama inavyoonekana hapa chini:

1. Jina la Shule: Shule ya Msingi ya Minga

Mradi: Ujenzi wa Shule mpya 1 yenye vyumba vya madarasa 16, matundu 18 ya vyoo, madarasa mawili ya awali na matundu 4 ya vyoo.

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 493,400,000

Fedha tumika hadi sasa: 322,408,406.19

Fedha salia: 170,991,593.81

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ujenzi, hatua ya kenchi, na upigaji lipu.

- Vyumba vya madarasa 12 hatua ya upauaji na lipu inaendelea.
- Jengo la utawala levo ya madirisha.
- Matundu ya vyoo 18 boma limekamilika.
- Madarasa 02 hatua ya kenchi, lipu inaendelea ndani na nje.



Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule mpya ya Minga ukiwa katika hatua za ukamilishaji.

2. Jina la Shule: Shule ya Msingi Nyerere

Mradi: Ujenzi wa Shule mpya 1 yenye vyumba vya madarasa 16, matundu 18 ya vyoo, madarasa 02 ya awali na jengo la utawala

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 493,400,000

Fedha tumika hadi sasa: 353,189,000

Fedha salia: 140,211,000

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ujenzi

- Vyumba 16 vya madarasa vimefikia hatua ya kupauliwa/ kuezwkwa bati.
- Vyumba 04 vya madarasa tayari wameanza plasta.
- Vyumba 02 vya madarasa wanajenga kozi za juu.
- Jengo la utawala limefikia hatua ya lenta.
- Matundu 18 ya vyoo wamwamwaga zege na shimo limefunikwa.



Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule Mpya ya Nyerere ukiwa unaendelea katika hatua ya upauaji.

3. Jina la Shule: Shule ya Msingi Mwaja

Mradi: Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa na matundu 3 ya vyoo

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 74,100,000

Fedha tumika hadi sasa: 71,478,630

Fedha salia: 2,621,630

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

- Vyumba 03 vya madarasa vimekamilika kupakwa rangi, wanaendelea kuweka vigae.
- Matundu 03 ya vyoo vimepauliwa, vipo hatua ya kupigwa plasta.



Mwonekano wa jengo la vyumba 03 vya madarasa shule ya msingi Mwaja vikiwa katika hatua ya uwekaji vigae na matundu 03 ya vyoo hatua ya plasta.

4. Jina la Shule: Shule ya Msingi Mnung'una

Mradi: Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa na matundu 4 ya vyoo

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 98,800,000

Fedha tumika hadi sasa: 85,490,040

Fedha salia: 13,309,960

Hatua ya Utekelezaji:

- Vyumba 04 vya madarasa ujenzi upo hatua ya upigaji plasta ndani na nje, pia vimeshapauliwa.
- Matundu 4 ya vyoo yapo hatua ya boma.



Mwonekano wa vyumba 04 vya madarasa shule ya Msingi Mnung'una vikiwa katika hatua ya upigaji plasta ndani na nje, pia yamepigwa boksi yakisubiri kupauliwa.

5. Jina la Shule: Shule ya Msingi Unyakhae

Mradi: Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 3 ya vyoo

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 74,100,000

Fedha tumika hadi sasa: 70,020,000

Fedha salia: 4,080,000

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

- Vyumba 03 vya madarasa hatua ya 'skimming'.
- Matundu 03 ya vyoo matungulizi yamekamiliwa, upauaji unaendelea.



Vyumba 03 vya madarasa shule ya Msingi Unyakhae vikiwa hatua ya skimming, na matundu 03 ya vyoo upauaji unaendelea.

6. Jina la Shule: Shule ya Msingi Manga

Mradi: Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 3 ya vyoo

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 74,100,000

Fedha tumika hadi sasa: 69,418,566

Fedha salia: 4,681,434

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

- Vyumba 03 vya madarasa hatua ya uwekaji plasta.
- Matundu 03 ya vyoo vipo hatua ya lenta, shimo limeshachimbwa.



Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa shule ya Msingi Manga ukiwa ktika hatua ya upigaji plasta na matundu 03 ya vyoo yakiwa hatua ya lenta.

7. Jina la Shule: Shule ya Msingi Manguanjuki

Mradi: Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa ya awali

Tarehe: 23 Juni, 2023

Fedha pokelewa: 63,600,000

Fedha tumika hadi sasa: 44,165,740

Fedha salia: 19,434,260

Hatua ya Utekelezaji: Ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

- Vyumba 02 vya madarasa hatua ya 'skimming'.
- Matundu 02 ya vyoo hatua ya lenta na shimo la choo limejengwa kutoka chini.
- Fensi imefikia kozi ya tano



Ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa shule ya awali ya mfano ya Manguanjuki, ukiwa katika hatua ya 'skimming' na matundu ya vyoo yakiwa hatua ya lenta.